

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

25 MEI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE – TAREHE 25 MEI, 2017

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

273. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA (MTAMBWE)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wananchi wengi Wajasiriamali huwa hawapati mikopo katika Taasisi za Fedha kwa sababu hawana uzoefu na ujuzi wa kutayarisha andiko la uchanganuzi wa miradi ya kibiashara pia hawana mali ya kuwawezesha kuweka dhamana:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaweka mpango madhubuti unaotekelezeka ili Wananchi hao waweze kukopesheka;
- (b) Je, Serikali haioni muda umefika sasa kuzitaka Taasisi za Fedha kupunguza

masharti ya ukopeshaji ili Wajasiriamali waweze kupanua miradi yao na kuwapatia ajira watu wengine.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

274. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kuna mjenzi aliyejenga Vituo vya Polisi kupitia Kampuni iitwayo Al Batna Building Co. Ltd. Vituo alivyojenga ni Kituo cha Polisi Mkokotoni – Unguja na Kituo cha Polisi cha Madungu kilichoko Chakechake Pemba kwa gharama ya Sh. 223,440,000/=:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa deni hilo la tangu mwaka 2012 hadi leo hii;
- (b) Je, Serikali inayo taarifa kwamba mwenye Kampuni hiyo, aliyejenga Vituo hivyo amepata maradhi makubwa huku akihangaika kufuatilia haki yake hiyo bila mafanikio;
- (c) Je, ni lini Serikali itamtembelea na kumpa pole kwa maradhi hayo mabaya yaliyompata.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

275. MHESHIMIWA JANET ZEBEDAYO MBENE (ILEJE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Wilaya ya Ileje ni kati ya Wilaya zinazozalisha sana mazao mbalimbali ya nafaka pia ina fursa nyingi sana za kilimo cha Cocoa, Vanilla, Tangawizi, Iliki na Pilipili Manga lakini hakuna viwanda vidogo na vya kati ili kuongeza thamani ya mazao hayo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha viwanda hivyo ili kuongeza ajira kwa Wananchi na pia mapato ya Serikali.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

276. MHESHIMIWA LUCY SIMON MAGERELI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Askari wa Jeshi la JWTZ wamekuwa wakijichukulia Sheria mikononi kwa kutesa raia na saa nyingine Askari wa Jeshi la Polisi. Matukio haya yamekuwa yakifanyika maeneo ya starehe, kwenye foleni za magari, mitaani na katika magari ya usafiri wa Umma; Hivi

karibuni Mkoani Tanga kijana mmoja kondakta wa daladala alimzuia mtoto wa Mwanajeshi kupanda daladala yake bila nauli, kondakta huyo alikamatwa na kuteswa na Wanajeshi ndani ya Kambi kitu kilichopelekea kifo chake:-

- (a) Je, Sheria ipi inawapa Wanajeshi haki kutesa raia;
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha hali hii.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

277. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Serikali inazuia Wavuvi kuvua samaki wadogo na hivyo nyavu zenye matundu madogo haziruhusiwi; katika Ziwa Victoria kuna samaki ambao kwa maumbile yao hawawezi kuwa wakubwa kama vile dagaa, furu na hata sato:-

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuzuia tu nyavu ndogo samaki hawa hawatavuliwa kamwe.


IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.



**DODOMA
25 MEI, 2017**



**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**